



HAKUNA SHUGHULI ZINAZOHUSIANA NA MAKAZI MAPYA (UHAMIAJI WA NCHI YA TATU) KWA SABABU YA UGONJWA WA COVID-19 (CORONA VIRUS), HADI MAELEKEZO MAPYA ZAIDI

Kufuatana na usambaaji wa ugonjwa ya COVID-19 (Virusi vya Corona) ulimwenguni, **hakutakuwa na shughuli za uhamiaji wa nchi ya tatu (makazi mapya) hadi maelekezo mapya yatolewe.**

Hii inamaanisha hakutakuwa na mahojiano (interviews) ya kwenda nchi ya tatu (na shirika la UNHCR na nchi ZOTE za tatu), hakuna ushauri wa kuhusu uhamiaji wa nchi ya tatu, hakuna mafundisho ya maisha, mila na desturi ya kuhusu nchi za tatu (Cultural Orientation), hakuna kutuma wagonjwa kwenye uchunguzi au vipimo vya hali ya afya (MAF) kwenye shirika la uhamiaji (IOM, OIM) na hakuna safari za kwenda kwenye nchi za tatu.

COVID-19 (Virusi vya Corona) imebaki kuwa tishio la ulimwengu na nchi nyingi zimesimamisha safari za kimataifa na mikutano ya kijamii. UNHCR imechukua uamuzi wa kusimamisha shughuli zote za uhamiaji wa nchi ya tatu (makazi mapya) kufuatana na maelekezo yaliyotolewa na muheshimiwa Rais wa Uganda tarehe 18 Machi 2020 ya kusimamisha mikutano ya kijamii.

UNHCR itawajulisha wakati shughuli na huduma za uhamiaji wa nchi ya tatu zitarudi kikawaida.

Hata kama umekubaliwa na nchi ya tatu, usiuze mali yako ya kibinansi.

Tafadhali fahamu kwamba ni shirika la UNHCR peke yake ambalo linahusika na shughuli ya uhamiaji wa nchi ya tatu (makazi mapya) nchini Uganda. Hakuna shirika la kimataifa au la taifa, kitengo cha serikali ya Uganda (kwa mfano, OPM), mwananchi wa Uganda au mkimbizi anayeweza kukusaidia kupata uhamiaji wa kwenda nchi ya tatu.

UNHCR ingependa kukumbusha wakimbizi wote kwamba huduma zote za UNHCR ni **ZA BURE**. Hakuna pesa au upendeleaji unaostahili kuombwa ili kupata huduma za UNHCR, ikiwepo msaada wa uhamiaji wa nchi ya tatu.

Kama umewasiliana na mtu ye yeyote anayekuahidi kuwa na uwezo wa kukuwezesha kupata huduma za uhamiaji wa nchi ya tatu (makazi mapya) kwa malipo fulani au kwa mabadilishano ya huduma nyingine, tafadhali toa ripoti kwa:

IGO: inspector@unhcr.org au Laini ya Usaidizi kwa Wakimbizi: helpline.uganda@unhcr.org au 0800 32 32 32

Kama una swalii au ulizo kuhusiana na kesi (dossier) yako ya uhamiaji wa nchi ya tatu (makazi mapya), tafadhali piga simu kwenye namba ya usaidizi kwa wakimbizi: 0800 32 32 32.